JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

(OR-TAMISEMI)

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA

NA

WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)

TARATIBU ZA USIMAMIZI WA KAZI

KATIKA

MPANGO WA MAENDELEO YA BARABARA KWA USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UFUNGUAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI P164920

RASIMU YA TAARIFA

FEBRUARI, 2021

MUHUTASARI WA KIUTENDAJI

Taratibu za Usimamizi wa Kazi zinajumuisha Sera, Kanuni, Sheria ndogondogo, Taratibu na uwezo ambavyo vinasimamia wafanyakazi (wenye ujuzi, wenye ujuzi kidogo na wasio na ujuzi) katika Taasisi/Wakala. Jamii inatarajia Serikali iwe na mifumo iliyoandaliwa ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaweza kufanya kazi zao kwa usalama. Sheria zinatungwa ili kudhibiti usimamizi wa vihatarishi vilivyoko katika sehemu za kazi; kuchunguza matukio ya vifo au kuumia katika sehemu za kazi; na kushtaki au vinginevyo kushughulikia tendo lolote lisiloendana na utaratibu uliowekwa.

Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi unatarajiwa kutumia rasilimali watu kutoka serikalini na ile itokanayo na mikataba. Ili kustawisha manufaa ya Mpango huu, Serikali ya Tanzania kupitia mawakala wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi, yaani TARURA na TANROADS inatambua umuhimu wa kuweka mazingira ya kazi salama na yenye afya, mahusiano bora kati ya mfanyakazi na uongozi, haki sawa kwa wafanyakazi, na ukuzaji wa usawa wa kijinsia na ulinzi kwa wanawake dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

Lengo la Programu hii ni kuboresha upatikanaji wa barabara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika maeneo ya vijijini yaliyochaguliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kujumuisha mbinu za ushirikishwaji wa jamii.

Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi una vipengele vinne (4):

- Kipengele cha 1: Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Vijijini
- Kipengele cha 2: Uimarishaji wa Taasisi na Rasilimali Watu
- Kipengele cha 3: Uhusishwaji, Ushirikishwaji na Ulinzi wa Jamii
- Kipengele cha 4: Ushughulikiaji Matukio ya Dharura

Kwa kuzingatia Sheria za Nchi na Viwango vya Kimazingira na Kijamii – Na. 2 (ESS2) ya Miongozo ya Kijamii na Kimazingira wa Benki ya Dunia, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini na Wakala wa Barabara Tanzania waliandaa Taratibu za Usimamizi wa Kazi ambazo zitatumika kuainisha mahitaji makuu ya wafanyakazi na hatari zinazohusiana na mpango huu pamoja na kubainisha rasilimali muhimu zitakazotumika kushughulikia masuala ya wafanyakazi wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Waraka huu wa Taratibu za Usimamizi wa Kazi wa Kudumu ulianzishwa wakati wa maandalizi ya Mpango huu na unadurusiwa na kuboreshwa wakati wote wa uendelezaji na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi.

Taratibu za Usimamizi wa Kazi zimeandaliwa kwa makusudi ili: kusaidia kusimamia usalama na afya katika maeneo ya kazi; kusimamia utoaji wa haki bila upendeleo, ubaguzi na kutoa fursa sawa kwa wafanyakazi wote wa mradi; kulinda wafanyakazi wa mradi ikiwa ni pamoja na wafanyakazi walio katika uhatarishi kama vile wanawake, watu wenye ulemavu, watoto (wa umri wa kufanya kazi, kwa kuzingatia ESS2) na wafanyakazi wahamiaji, wafanyakazi wa mikataba na wafanyakazi wasambazaji; kuzuia aina zote za matumizi ya wafanyakazi wanaolazimishwa na watoto; kuunga mkono kanuni za uhuru wa ushirikiano na majadiliano ya pamoja ya wafanyakazi wa mradi katika namna inayoendana na Sheria za Kazi za Nchi, kanuni na Viwango Na. 2; na kuandaa Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko ili wafanyakazi wa mradi waweze kupeleka matatizo yao.

Wafanyakazi watakaohusika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi ni: wafanyakazi wa moja kwa moja, wafanyakazi wa mikataba pamoja na wafanyakazi wahamiaji. Uhakika wa mazingira mazuri ya wafanyakazi na mazingira mazuri ya kazi kwa watu wote wataohusika katika utekelezaji wa Mpango huu umepewa kipaumbele cha juu na TARURA na TANROADS. Taratibu za Usimamizi wa Kazi zinapaswa kutekelezwa na pande zote zinazohusika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Hatari zinazoweza kujitokeza zimebainishwa na zinajumuisha hatari za kiusalama na afya (mf. ajali na kuumia), uwezekano wa matukio ya kutumikisha watoto, wingi wa wafanyakazi, hatari za Unyanyasaji wa Kijinsia na uwezekano wa maatukio mapya ya maambukizi ya VVU/Ukimwi.

Ili kuimarisha utendaji bora, kuinua ufanisi na kukidhi mahitaji ya kijamii na kimazingira, Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi ulizingatia mahitaji ya kisheria na kikanuni ya Tanzania, Sera na Viwango vya Benki ya Dunia pamoja na Shirika la Kazi Duniani zinazohusu usimamizi wa wafanyakazi. Kwa kutumia sheria za nchi mahususi, Utaratibu huu wa Usimamizi wa Kazi unazingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Tanzania ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi (sheria ndogo) na kanuni zinazoambatana nazo kwa ajili ya kulinda usimamizi na haki za wafanyakazi. Aidha, Sheria hiyo inadhibiti masuala ya ajira kwa kuzingatia viwango vya ajira. Wakati huohuo, Sheria ya Namba 5 Afya na Usalama Kazini ya mwaka 2003 (Sehemu ya IV Kifungu cha 43 Masharti ya usalama; Sehemu ya V kifungu cha 54, 55 na 58 Masharti ya Afya na Ustawi; Sehemu ya VI Kifungu cha 61 (1a), 63(a,b), na 65 Masharti Maalumu ya Sheria), inaeleza taratibu kwa ajili ya kulinda usalama, afya na ustawi wa watu wasio wafanyakazi katika maeneo ya kazi. Kwa upande mwingine, Mwongozo wa Kijamii na Kimazingira wa Benki ya Dunia (ESF), Viwango Na. 2 vya Kijamii na Kimazingira vinatoa mwongozo ulio wazi kuhusu wafanyakazi na mazingira ya kazi. Viwango vya Wafanyakazi vya Shirika la Kazi Duniani ambapo Tanzania ni mwanachama vinajumuisha: Kifungu cha 29 (makubaliano ya kazi za shuruti); Kifungu cha 87 (makubaliano ya uhuru wa kujumuika na ulinzi na haki ya kuunda chama cha wafanyakazi); Kifungu cha 98 (makubaliano ya haki ya kupanga na kuafikiana kwa

pamoja); Kifungu cha 100 (makubaliano ya malipo sawa); Kifungu cha 105 (makubaliano ya kukomesha kazi za shuruti); Kifungu cha 111 (Makubaliano kuhusu Ubaguzi katika Ajira na Kazi); Kifungu cha 138 (Makubaliano kuhusu Umri wa Chini); na Kifungu cha 182 (Makubaliano kuhusu aina mbaya kabisa za matumizi ya watoto katika kazi).

Mawakala wa utekelezaji wa Mpango huu wanapaswa kuhakikisha kuwa wakandarasi wanaandaa utaratibu wa kushughulikia malalamiko kwa wafanyakazi wao ikiwa ni pamoja na wakandarasi wadogo pamoja na jamii kwa ujumla ili kutatua matatizo ya sehemu za kazi na jamii. Kwa shughuli za ukarabati wa barabara ambazo hazitahusisha mkandarasi, kutakuwa na mtu maalumu ndani ya vitengo vya utekelezaji wa mradi (PIU) atakayekuwa akishughulikia malalamiko yote.

Malalamiko yanaweza kutolewa bila mhusika kujulikana na yatapitiwa kila baada ya juma moja yakifuatiwa na uchukuaji wa hatua ya kurekebisha ndani ya siku mbili kwa malalamiko ambayo ni muhimu zaidi. Ikiwa mgogoro utashindwa kupatiwa ufumbuzi kwa kutumia utaratibu wa kushughulikia malalamiko wa mkandarasi, kutakuwa na fursa kwa wafanyakazi kuwasilisha malalamiko yao kwa Kamati inayoshughulikia Malalamiko ya Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi katika ofisi za Waratibu wa Mikoa wa TARURA na TANROADS kisha yataenda kwa mtu anayesimamia Vitengo vya Utekelezaji wa Mradi (PIU). Vitajumuishwa vifungu mahususi vinavyohusiana na malalamiko ya Ukatili na Unyanyasaji wa Kingono yatakayotokana na mradi ili kuhakikisha kuna faragha na haki ya mwathirika inalindwa. Utaratibu wa malalamiko wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi hautawazuia wafanyakazi kutumia taratibu za kutatua migogoro zilizowekwa katika sehemu ya VIII ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Taratibu za Usimamizi wa Kazi ni muhimu na za lazima kwa sababu zinasaidia kufafanua masuala ya wafanyakazi na mazingira ya kazi na namna yanavyowaathiri wafanyakazi pamoja na jamii kwa ujumla. Mawakala wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi watasaidia kuweka mazingira salama katika maeneno ya kazi; kuzuia au kupunguza rushwa, mwenendo mbaya na uongozi mbaya wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi.

Katika utekelezaji wa ESS 10, mashauriano na wadau husika yalifanyika wakati wa maandalizi ya LMP na nyaraka nyingine za miongozo (kwa mfano SEP, VGPF, ESMF, RPF, ESCP). Mkopaji aliandaa warsha kadhaa za ushauri kwa umma katika ngazi za mikoa na kitaifa ili kuongoza maandalizi na kuwafahamisha kuhusu nyaraka sita (6) za mradi. Jedwali ES-1 hapa chini linaonyesha orodha ya mashauriano yaliyofanywa wakati wa maandalizi ya nyaraka (ESF) za mradi wa RISE.

Jedwali ES-1: Orodha ya Mashauriano wakati wa maandalizi ya mradi wa RISE

Na	Jina la mashauriano	Eneo	Idadi ya waliohudhuria	Tarehe
1	Warsha ya Kitaifa ya Wadau.	Mkoani Dodoma	73	Januari 09 2020
2	Mashauriano ya Wadau Kitaifa - maalum kwa ajili ya VGPF	Mkoani Dodoma	5	Januar1 21, 2020
3	Mashauriano ya Wadau Kimkoa - maalum kwa ajili ya VGPF	Mikoani Morogoro, Dar es Salaam & Dodoma	16	Februari 07 mpaka 11 2020
4	Mashuriano na Wadau wa Mkoa wa Iringa.	Mkoani Iringa	05	Machi 10 2020
5	Jukwaa la Wadau la Webinar Kitaifa.	Mkondoni	11	April 02, 2020
6	Mashuriano na Wadau wa Mkoa wa Lindi.	Mkoani Lindi	20	Januari 05 2021
7	Mashuriano na Wadau wa Mkoa wa Tanga.	Mkoani Tanga	34	Januari 05 2021
8	Mashuriano na Wadau wa Mkoa wa Geita.	Mkoani Geita	33	Januari 08 2021
9	Jukwaa la Wadau la Webinar Kitaifa.	Mkondoni	23	Januari 13 2021

Maelezo ya mashauriano husika kwa nyaraka za ESF yanapatikana katika Kiambatisho I cha SEP ya RISE. Maoni kutoka kwa warsha ya mashauriano yameingizwa katika nyaraka husika za mradi.